

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anwani ya Simu: "REGCOM"
Simu ya mdomo: (028) 2220215-18
E-mail: ras.kagera@tamisemi.go.tz
Fax: (028) 2222341 / 2221356



**OFISI YA MKUU WA MKOA,
S. L. P. 299,
BUKOBA - KAGERA.
TANZANIA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
TAREHE 26 MEI, 2017**

Ndugu Waandishi wa Habari, Kupitia kwenu napenda kutoa taarifa kwa umma hasa kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera kuhusu Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa inayoadhimishwa Kitaifa hapa Mkoani kwetu katika Uwanja wa Kyakailabwa nje kidogo ya mji wa Bukoba kuanzia tarehe 28 Mei, 2017 hadi tarehe 1Juni, 2017.

Ndugu Waandishi wa Habari, Malengo ya Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa Kitaifa inalenga kuelimisha wananchi na umma juu ya matumizi ya maziwa kama chakula bora kwa watu wa rika zote na faida za maziwa katika kujenga afya ya binadamu. Umuhimu wa maziwa katika lishe na afya bora ya binadamu unatokana na kuwa ni chakula kamili kinachojitegemea kwa kuwa na viinilishe vyote muhimu vinavyohitajika mwilini kwa pamoja.

Ndugu Waandishi wa Habari, Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa Mkoani Kagera yatakuwa na dhana ya kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa maziwa na kutoa fursa kwetu sisi viongozi kuwahamasisha wadau na wananchi kuongeza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ili kuondoa umasikini na kuongeza lishe. Katika Mkoa wa Kagera kwa sasa kuna idadi ya ng'ombe wa maziwa **21,438** ambapo unywaji wa maziwa kwa mtu mmoja kwa mwaka katika Mkoa wa Kagera ni **lita 16** tu ukilinganisha na unywaji wa maziwa kwa mtu mmoja kwa mwaka Kitaifa ambapo ni **lita 47**.

Ndugu Waandishi wa Habari, Unywaji wa maziwa Kimkoa na Kitaifa nilioutaja hapo juu bado hauendani na kiwango cha unywaji wa maziwa Kimataifa ambapo mtu mmoja anatakiwa kunywa maziwa **lita 200** kwa mwaka. Kwa takwimu hizo bado unywaji wetu wa maziwa upo katika kiwango cha chini sana ambapo wananchi wanahitaji sana elimu juu ya unywaji wa maziwa na kupitia Maadhimisho haya elimu hiyo itatolewa ili tunywe maziwa kwa faida zetu wote.

Ndugu Waandishi wa Habari, Katika upatikanaji wa maziwa kwenye Mkoa wetu wa Kagera kwa mwaka 2014/2015 mkoa ulizalisha maziwa **lita 43,915,266**. Mwaka 2015/2016 mkoa ulizalisha maziwa **lita 46,858,481**. Mwaka 2016/2017 Julai hadi Desemba mkoa ulikuwa umezalisha **lita 21,141,709** ambapo kiwango hicho kilishuka kutokana na ukame uliokuwa umeukumba Mkoa wetu wa Kagera. Pamoja na uzalishaji huo wa maziwa bado kiwango hicho hakitoshelezi kwenye mkoa jambo ambalo nalitolea wito kwa wafugaji kushiriki kikamilifu katika maadhimisho haya ili kupata elimu ya kutosha itakayowafanya wafuge kisasa na kuinua kiwango cha uzalishaji wa maziwa katika Mkoa.

Ndugu Waandishi wa Habari, Natoa wito kwa wananchi wote (watu wazima pamoja na watoto) wa Mkoa wa Kagera kuhudhuria kwa wingi kuanzia tarehe 28 Mei, 2017 siku ya ufunguzi hadi tarehe 1 Juni, 2017 siku ya kufunga katika Uwanja wa Kyakailabwa kupata elimu ya unywaji wa maziwa, ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa, usindikaji wa maziwa pamoja na mazao yake, na faida za unywaji wa maziwa kwa ujumla.

Pia wananchi watajionea wenyewe bidhaa mbalimbali zinazozalishwa kutokana na maziwa kwenye mabanda mbalimbali ya wadau wa ufugaji na wasindikaji wa Maziwa. Vilevile kwa wananchi watakaohudhuria katika maadhimisho hayo watapata fursa ya kunywa maziwa yatakayokuwa yanapatikana uwanjani kwa wingi kila siku kuanzia siku ya ufunguzi hadi siku ya kilele.

Ndugu Waandishi wa Habari, Maadhimisho hayo yatahudhuriwa na Viongozi wa Kitaifa ambao watashiriki pamoja nasi katika ufunguzi, wakati wa maadhimisho na wakati wa kufunga maadhimisho hayo. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ni **“Kunywa Maziwa Furahia Maisha”**. Maadhimisho haya yatakuwa ya 20 mfululizo kuadhimishwa nchini ambapo yalianza kuadhimishwa kuanzia mwaka 1998 na mwaka jana yaliadhimishwa Mkoani Njombe.

Aidha, Wiki ya Maziwa ilianzishwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) ambao waliichagua Wiki ya mwisho wa mwezi Mei kila mwaka kuwa ndiyo Wiki ya Uhamasishaji wa Unywaji wa Maziwa Duniani kwa kuzingatia kuwa maziwa ni chakula bora kwa watu wa rika zote na ni mlo ulio kamili.

Ndugu Waandishi wa Habari, *Mwisho*, nipende kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuhudhuria Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa Mkoani kwetu katika Uwanja wa Manispaa ya Bukoba kama ambavyo tumekuwa na utamaduni wa kushiriki katika matukio mbalimbali kwa pamoja. Pia katika Maadhimisho hayo kutakuwa na ulinzi wa kutosha kwani vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vimejipanga vizuri kuhakikisha tunaadhimisha Wiki ya Maziwa kwa amani, upendo na utulivu wa kutosha.

“Kunywa Maziwa, Furahia Maisha”

Imetolewa na; Mhe. Meja Jenerali (Mst) Salum M. Kijuu,
Mkuu wa Mkoa,
KAGERA.